Kiswahili Activities - Grade 3 Term 1 Exam 2023

1. SEHEMU YA 1
   KUZUNGUMZA NA KUSIKILIZA
   a. Habari ya asubuhi?
      (mwanafunzi kujibu)
   b. Mnasoma gredi la ngapi?
      (mwanafunzi kujibu)
   c. Mnapenda mchezo gani?
      (mwanafunzi kujibu)
   d. Jina la mwalimu mkuu?
      (mwanafunzi kujibu)

2. SEHEMU YA 2
   KUSOMA
   Alama za barabarani ni muhimu. Watu wanaendesha magari wanastahili kuzingatia alama hizo. Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule. Wanaotumia barabara wanafaa kuwa waangalifu wanapokiona. Ni hatari kwa watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine na herufi H inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo ni lazima awe mwangalifu na apunguze kasi ya gari lake vilevile, haruhusiwe kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama nyingine ni kuvukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa, ajali hupungua.

3. SEHEMU YA 3
   Soma kifungu kisha ujibu maswali
   Shule yetu inaitwa Bonda ina madarasa manane na wanafunzi mia tano hamsini. Walimu wetu ni tisa. Walimu hawa hufanya kazi ya ualimu yaani kufundisha wanafunzi. Mwalimu mkuu ni Bwana Juma Koyana. Yeye ndiye msimamizi mkuu wa shule. Bi Chebet ni naibu mwalimu mkuu. Yeye humsaidia mwalimu mkuu kusimamia shule haswa katika upande wa nidhamu. Bi Chebet, pia ni mwalimu wa darasa letu. Yeye hapendi wanafunzi wanaorandaranda ovyo darasani.

   Kiranja wa darasa letu anaitwa Zafani Mwongera. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii za mchwa na hufanya vyema darasani. Siku moja, wakati wa mvua hakuweza kubeba vitabu kumpelekea mwalimu.

1. Maswali
   a. Shule ya msimulizi inaitwa aje?
      _____
   b. Jina la mwalimu mkuu ni?
      _____